



BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 30 Mei, 2022

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. TAARIFA YA SPIKA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Mawasiliano, Ardhi na Nishati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa Mwaka 2022/2023.

III. MASWALI:

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:

152. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Je, Wizara kupitia BAKIZA haioni kwamba ipo haja ya kuwepo kwa kamusi la kiswahili na uchumi wa buluu.

Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

108. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Kwa kuwa barabara ya Ole-Kengeja imeunganisha mikoa yote miwili ya Pemba, na kwa kuwa kuanzia Ole- Kianga hadi kufika Kengeja barababara hii ina sehemu nyingi za mipindo mikali, kalavati pamoja na madaraja bila kuweka alama za barabarani zinazoonesha uwepo wa mipindo (cross) pamoja na madaraja.

Je, ni lini Serikali katika kuepusha ajali itaweka alama zitakazomuonesha dereva uwepo wa madaraja na mipindo mbele yake.

125. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Ni jambo la kufurahisha kwamba Serikali ya awamu ya nane ilibuni mpango mpya wa kuzijenga na kuziimarisha barabara kuu na barabara za ndani katika visiwa vya Unguja na Pemba, mpango ambao uliahidiwa kuanza ndani ya mwaka wa fedha 2021/2022. Hata hivyo, kumekuwa na taarifa chache kuhusiana na mpango huo.

- (a) Je, Serikali imepata mkopo au mfadhili gani kwa ajili ya mpango huo.
- (b) Je, ni barabara ngapi za ndani na ngapi kuu Unguja na Pemba ambazo zimeshaanza kujengwa na ujenzi umefikia wapi.
- (c) Je, ni mkandarasi yupi, mshauri elekezi yupi na kwa gharama zipi katika mkataba wa mpango huo unaotekelezwa.

Wizara ya Afya:

105. MHESHIMIWA SAID SALEH SALIM (Jimbo la Tumbe) -
Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Wananchi wa Tumbe wanaishukuru sana Serikali kwa kukubali na kushirikiana nao katika ujenzi wa Kituo cha Afya cha mama na mtoto.

- (a) Je, ni lini Wizara itakifungua kituo hicho ili kuwapunguzia usumbufu wananchi hao hasa akina mama na watoto.
- (b) Kwa kuwa katika kituo hicho cha asili kina matatizo ya uhaba wa dawa je, ni sababu zipi zilizopelekea ukosefu huu wa dawa.

Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

142. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Miongoni mwa shughuli kubwa za wananchi wa jimbo la Pandani ni uvuvi mdogo mdogo ufanywao katika bahari ya ukanda wa mashariki mwa vijiji vya Kiungoni, Mjananza na Shengejuu. Hata hivyo, bado wavuvi wadogo wadogo wa jimbo la Pandani hawana nyenzo za uvuvi na wana hali duni ya kumudu kununua nyenzo hizo.

- (a) Je, ni lini Serikali itawapatia wavuvi wa jimbo la Pandani boti za uvuvi ndogo ndogo za watu 30 hadi 50 kwa njia ya ruzuku au mkopo.
- (b) Je, ni upi utaratibu unaotakiwa kufuatwa na wavuvi kuweza kupata boti za uvuvi ndogo ndogo kwa njia ya ruzuku au mkopo.
- (c) Je, boti ndogo ndogo zinazopangwa kununuliwa na Serikali zinagharimu kiasi gani na zinatarajiwa kuwa na umri gani kwa wastani.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

177. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani)
- Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali itakumbuka kwamba mnamo mwaka 1950, Haji bin Miaka Shirazi na Bakari bin Miaka Shirazi walinunua shamba kutoka kwa Mussa bin Zaid Mzigua Mikindani/Tungamaa. Hata hivyo, inasikitisha kwamba sehemu ya shamba hilo imegeuzwa *dampo* la kutupia taka tokea mwaka 1972 ambapo Chuo Cha Mafunzo waliliazima bila kuandikiana na warithi wa shamba hilo. Shamba lile limenyang'anywa na mtu mwingine kwa kushirikiana na Serikali.

- (a) Je, ni lini Serikali itakiamuru Chuo Cha Mafunzo kutoendelea kulifanya dampo shamba hilo.
- (b) Je, ni lini Serikali itamuamrisha aliyenyang'anya shamba hilo mwaka 2015 kuwacha kulitumia shamba hilo.
- (c) Je, ni kwa nini hata baada ya zuiro lililotoka aliyenyang'anya aliendelea kuchuma karafuu na zilipoisha Serikali ikalikodisha shamba hilo.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

Waziri wa Ardhi na Maendeleo ya Makaazi:

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi kwa mwaka 2022/2023.

Zanzibar,
30 Mei, 2022.


(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA